

Kulikuwa na basi moja tu katika kijiji cha Ebei. Lilikuwa basi kubwa lenye rangi ya bluu. Lilinguruma sana.



Siku moja mamake Ebei alisema, “Kesho tutaenda mjini kununua sare yako ya shule.”



Ebei alifurahi sana.
Kumbe atasafiri katika
lile basi kubwa la bluu!
Usiku huo hakuweza
kulala vizuri.



Mamake alipoenda kumuamsha, Ebei alikuwa tayari amevaa.



Ebei na mamake walienda kwenye kituo cha basi. Walisubiri lile basi kubwa la bluu. Basi halikufika.



Watu wengine walifika kwenye kituo cha basi. Wote walilalamika kuwa basi lilichelewa. Mmoja aliuliza, "Basi limetuacha?"

Ebei alikuwa na wasiswasi.
“Tusipokwenda mjini, sitapata sare
yangu ya shule,” aliwaza.






Baadhi yao walikata tamaa wakarudi nyumbani. Lakini Ebei alilia akakataa kurudi. "Tutasubiri zaidi," mamake alimtuliza.



Ghafla, walisikia mngurumo. Wakaona vumbi hewani. Basi lilikuwa linakuja kwa kasi.




Basi halikuwa la bluu
wala halikuwa kubwa.
Basi lile lilikuwa dogo
na jekundu.
Waliosubiri
waliliangalia tu na
hawakuingia ndani.



Dereva aliwaita,
“Ingieni! Ingieni!
Tumechelewa sana
leo.”



Ebei na mamake walikuwa wa kwanza kuingia. Mara wote waliingia ndani ya basi lile dogo jekundu.



Ebei alichungulia dirishani. Aliwaona watu wengi zaidi wakiingia ndani ya basi.



Mara basi likaondoka.
Ebei aliwaona watu
wengine wakikimbia
kulifikia basi. Walikuwa
tayari wamechelewa.



Mamake Ebei alimuuliza dereva, “Liko wapi basi kubwa la bluu?” Dereva alimjibu, “Samahani mama, basi la bluu liliharibika. Linatengene Kesho litakuja.”



Ebei hakujali rangi wala ukubwa wa basi. Alifurahi kuwa basi lile lilikuwa linawapeleka mjini. Hatimaye, atanunuliwa sare ya shule.